
# MKRISTO KATIKA ULIMWENGU ULIOJAA ROHO

# (MWALIMU)



BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

# MKRISTO KATIKA ULIMWENGU ULIOJAA ROHO

## (MWALIMU)

Kimeandikwa na Paul Kyalimpa Amooti, Josphat M.M. Gikiri
na Andrew Mwenge

**BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH**

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

Y1-4Ts

Used with permission of International Publications Services

Published by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

©Copyright, 1990
Baptist Publications House
All Rights Reserved

kulikariri. Neno la Mungu hubadili maisha yake. Mkristo huyo huongozwa na Roho Mtakatifu."

**KUOMBA**

1. Mwombee mwanafunzi ye yote ambaye hajampokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake.

2. Mwombe Roho Mtakatifu akutumie unapofundisha na pia wanafunzi wako waongozwe na Roho Mtakatifu.

3. Waombee wakae ndani ya Kristo kila siku.

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Uliza: "Je! wewe huongozajwe na Roho Mtakatifu?" Andika majibu yao ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Wanapaswa kusema kuupata uzima wa milele, kuunganishwa na Mungu, kuelewa Neno la Mungu, kupata amani ya Yesu, kumtii na kushinda majaribu."

Uliza: "Je! nini hufanyika unapotumbukiza chuma ndani ya maji?" Wape muda wa kujibu.

Sema: "Huzama kwa sababu ya sheria ya uvutano. Lakini chuma hicho kitaelea kikifunguwa kwenya mbao. Je, kwa nini?" Mmoja wao aeleze kwa ufupi.

Uliza: "Je! sheria ya dhambi inasemaje?" Waambie wafungue Warumi 6:23.

Sema: "Dhambi inastahili kufa, lakini uwezo wa Mungu umezidi dhambi zetu. Mungu yuko tayari kutusamehe dhambi zetu na kutufanya wenye haki tunapompokea Yesu kuwa Mwokozi."

Uliza:"Je! unawezaje kujua kwamba unaongozwa na Roho Mtakatifu?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema: "Kazi ya kwanza ya Roho Mtakatifu katika maisha ya mtu ni kumsaidia aweze kuokoka. Hutupa imani na ufahamu wa kuamini kwamba Yesu alifia dhambi zetu. Hatimaye hutusaidia kuishi kwa ajili ya Yesu kila siku. Hutuongoza katika njia zote tulizojifuna katika somo hili. Hutusaidia kufahamu umoja wetu na Mungu. Hutusaidia kuelewa Neno la Mungu, kumtii na kufahamu amani yake."

Waambi wanafunzi wafungue na wasome pamoja Yohana 15:7. Sema: "Kila Mkristo anayo haki ya kumwomba Mungu. Mungu ameahidi kusikia na kujibu sala zetu. Yule anayekaa ndani ya Kristo hutii Neno la Mungu. Hulisoma na kutafakari na



# YALIYOMO

**SURA** **UKURASA**


1. Shetani, Mwanzo na Kuanguka Kwake. . . . . . . . . . . . . . . 5
2. Shetani, Kazi Yake Siku Hizi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10
3. Shetani na Hukumu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 15
4. Uchawi na Kazi ya Shetani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .20
5. Jinsi ya Kutambua Uchawi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .26
6. Uchawi na Mkristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .31
7. Roho Mtakatifu na Utatu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .36
8. Roho Mtakatifu na Uongozi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 42
9. Kuja kwa Roho Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 46
10. Kazi ya Roho Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 51
11. Kujazwa na Roho Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 57
12. Roho Alifanyika Mwili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
13. Kuongozwa na Roho Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . .66

# KUHUSU WAANDISHI

Kitabu hiki kimeandikwa na Paul Kyalimpa Amooti, Josphat M.M. Gikiri na Andrew Mwenje. Walitumia kitabu cha International Publications Services chenye kichwa hiki kama msaada wa kuandika upya katika mtindo mpya.

Amooti ni mwinjilist huko Uganda. Ametumika kama mkurugenzi wa Bible Way Correspondence School katika nchi yake. Yeye ni mshiriki wa Kampala Baptist Church.

Gikiri ni mwalimu huko Maragua, Kenya. Yeye ni mshiriki wa Kaimiri Baptist Church, na anatoka Kenya.

Mwenge ni mchungaji wa vijana wa Kampala Baptist church ambako ni mshiriki.

ana uwezo wa kushinda dhambi. Kila Mkristo anaweza kupata uwezo huu. Hebu tujifunze Neno la Mungu ili tufahamu nguvu na uwezo huu."

**MAELEZO**

Soma Yohana 14:16-31. Sema: "Tumejifunza kwamba Roho Mtakatifu alikuwepo wakati wa uumbaji. Tumejifunza pia kwamba alikuwepo 'hapo mwanzo.' Roho Mtakatifu alikuja kuwasaidia watu maalum na wakati maalum katika Agano la Kale na wakati Yesu alipokuwa ulimwenguni.

"Yesu, katika vifungu hivi, aliwatayarisha wanafunzi wake kwa ajili ya kufa na kuondoka kwake kurudi mbinguni. Aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu kuishi ndani yao na kuwasaidia. Ilikuwa vigumu kuelewa yale waliyoambiwa na Yesu. Yesu aliwaambia pia kwamba hata ulimwengu hautaelewa. Wale tu waliomkubali Yesu ndio wangepewa na kusaidiwa na Roho Mtakatifu."

Uliza: "Je! inamaanisha nini kusema Mkristo anaongozwa na Roho Mtakatifu?"

Mwalimu, tumia maelezo ya Msingi wa Somo Hili kufundisha jinsi Roho anavyosaidia kama ilivyoandikwa katika vifungu vya 18-20. Kuna uzima wa milele na kuunganishwa na Mungu pamoja na waamini wengine. Endelea kueleza jinsi anavyosaidia,(vifungu vya 21-24) kumtii Yesu, kuelewa Neno la Mungu na kuwa na amani. Hutusaidia pia kupigana vita na Shetani anapokuja kutujaribu.

Sema: "Hii ndiyo sababu ni muhimu kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mmwokozi. Hakuna njia nyingine ya kupata uzima wa milele. Hakuna njia nyingine ya kuunganishwa na Mungu, wala kumtii au kuelewa Neno lake na kuwa na amani."

anayemwongoza kutii mafundisho ya Kristo. Soma Vifungu vya 25-27.

Roho humsaidia mwamini kuelewa Neno la Mungu. Roho Mtakatifu ni mwalimu wa mwamini. Huwakumbusha Wakristo mafundisho ya Yesu Kristo.

Roho huwapa Wakristo amani ya Yesu. Hii siyo amani ambayo ulimwengu unaweza kuuelewa. Mwamini hapati amani kwa kuepuka mateso. Bali huyakabili mateso kwa matumaini na msaidizi wake, Roho Mtakatifu. "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28). Mungu ana mpango wa ajabu kwa kila mwamini. Soma vifungu vya 28-31.

Roho humwongoza mwamini katika maisha ya ushindi. Shetani atakuja kumjaribu ili afanye dhambi. Lakini Roho yupo kumsaidia mwamini anayetaka msaada. Ni muhimu kwa Mkristo kuomba asije akafanya dhambi. Roho atamwongoza kushinda majaribu kama haya. Ni lazima Mkristo atii uongozi wa Roho Mtakatifu.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Anza kwa kumwambia mwanafunzi mmoja asome Utangulizi katika kitabu chake. Tumia vifaa ulivyoleta kuonyesha jinsi inavyofanyika.

Sema: "Tunaweza kumliganisha mwamini na vitu vinavyoelea majini pamoja na nguvu za uvutano. Anaweza kushinda dhambi hata kama akivutwa au akishawishiwa kufanya dhambi. Je! kwa nini? Ni kwa sababu anaongozwa na Roho Mtakatifu. Lakini Mkristo hufanya dhambi wakati mwingine. Udhaifu huu uko ndani yake wala si katika Roho Mtaktifu. Roho Mtakatifu



**SURA YA KWANZA**

# SHETANI, MWANZO NA KUANGUKA KWAKE

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Mwanzo 3; Ezekieli 28:12-18; Isaya 14:12-14

VIFUNGU VYA LEO: Ezekieli 28:12-18; Isaya 14:12-14.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Usishindwe na ubaya, bali uushide ubaya kwa wema" (Warumi 12:21).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kuhusu mwanzo na kuanguka kwa Shetani na yale anayoweza kuwafanyia.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Andika ubaoni maneno haya: Mwanzo na Kuanguka kwa Shetani.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Ezekieli alilinganisha mwanzo wa Shetani na mfalme wa Tiro. Ezekieli 28:12-18 inatuambia kuhusu tabia, mahali na cheo cha Shetani kabla ya kuanguka kwake. Hebu kwanza tuzungumzie asili au mwanzo wake.

Kifungu cha 12 kinaonyesha uhusiano uliokuwepo kati ya mfalme wa Tiro (Shetani) na Mungu. Uhusiano huu ulikuwa kamilifu. Mfalme huyu alikuwa mwenye hekima mkamilifu wa uzuri.

Je! Shetani alikuwa wapi? "Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu..." (kifungu cha 13). Adeni, bustani ya Mungu, ilikuwa na kila kitu ambacho Shetani alihitaji. Vitu hivi vilikuwepo hata kabla Shetani hajaumbwa. Palikuwa mahali pazuri na pakamilifu.

Kifungu cha 14 kinasema kwamba Mungu alimtia mafuta malaika mwingine kumchunga Shetani. Hii inaonyesha kwamba Shetani alikuwa mkuu wa malaika wa Mungu. Alitawala malaika wengine. Hii ndiyo kazi aliyofanya.

Kifungu cha 16 kinaonyesha mwanzo wa shida. Lusifa alianza kuwa na kiburi. Kifungu kinasema, "... watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi...." Hekima, mapenzi na mawazo ya Shetani yalianza kuwa mabaya. Alipoteza uzuri wake, na akaadhibiwa vikali sana. Alianza kujivuna badala ya kunyenyekea. Hii ilikuwa dhambi.

Je! alipewa adhabu gani? Vifungu vya 17-18 vinasema, "...nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama. Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza...." Vifungu hivi vinatuonyesha adhabu ya dhambi. Aliteketezwa na moto.

Isaya analinganisha kuanguka kwa Shetani na mfalme wa Babeli. Nabii huyu ametuambia katika Isaya 14:12-14 tamaa aina tano zilizomwangusha Shetani. Tamaa hizi zinaweza kuwafanya wanafunzi wako waanguke katika maisha yao ya Kikristo. Unapaswa kuwaonya wajihadhari.

Tunapata katika kifungu cha 12 jina la nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi. Shetani ndiye aliitwa jina hili. Ndiye ambaye Yesu alizungumzia aliposema, "...Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme" (Luka 10:18).

Vifungu vya 13-14 vinatuambia zile tamaa tano zilizomwangusha Shetani. 1. Alitamani kupanda mpaka mbinguni, 2. Alitaka kuinua kiti chake juu kuliko nyota za Mungu. 3. Alitaka kuketi juu ya mlima wa mkutano kama



kuwekelea chuma hicho. Andika ubaoni au kwenye karatasi kubwa maneno haya: Ninaongozwa na Roho Mtakatifu.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Tunaona katika Yohana 14:16-31 jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hutuongoza. Ni muhimu kuelewa maana ya neno la Kiyunani na Roho Mtakatifu kabla ya kufundisha sehemu zinazohusika. Neno hili, mshauri (mfariji au msaidizi), linamaanisha yule anayeitwa kusaidia wakati wa mahitaji.

Vifungu vya 18-20 vinatuonyesha sehemu mbili ambazo huwa tunaongozwa na Roho Mtakatifu. Hutuongoza kwanza katika uzima wa milele. Haya ni maisha yasiyo na mwisho ambayo kila mwamini hupokea anapomkubali Yesu. Yohana 3:16 inasema, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Maisha haya ni yale ambayo mwamini huishi ulimwenguni. Ni maisha ambayo humpendeza Kristo kuishi maisha haya.

Pili, Roho humwongoza kila mwamini katika ushirika mpya na Mungu. Mtu anapookoka hufanyika mwana wa Mungu. "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu..." (Yohana 1:12). Huu ndio uhusiano mpya ambao mwamini huanza. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kumwongoza mwamini katika ushirika huu. Roho humwonyesha mwamini umoja huu ambao upo kati yake na Mungu.

Tunaambiwa katika vifungu vya 21-24 kwamba Roho hutuongoza kumtii Yesu. Mungu humpa mwamini karama ya Roho Mtakatifu wakati anapookoka. "Nanyi pia katika huyo mmekwisha ...kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu" (Waefeso 1:13). Karama hii inathibisha kwamba yeye ni wa Mungu. Roho huwa msaidizi

"Roho Mtakatifu yupo kukupa nguvu kubadili tabia mbaya. Unaweza pia kutiwa nguvu na Roho uishi maisha matakatifu na ya haki mbele za Mungu.

"Yesu anatuita tujinyenyekeze na tuache dhambi zetu tuwe kama yeye, mtakatifu na msafi. Atatusaidia kufanya hivyo kama tutamwomba. Roho Mtaktifu hutusaidia kubadili mwenendo. Hutusaidia kufuata mfano wa Yesu badala ya kumfuata Shetani."

**KUOMBA**

1. Mwombe Roho Mtakatifu akuongoze unapofundisha.

2. Mwombe akusaidie wewe na wanafunzi wako kuwa wanyenyekevu.

3. Mwombe Roho Mtakatifu akusaidie pamoja na kuacha tabia mbaya ambazo ziko maishani mwenu.

## SURA YA KUMI NA TATU

# KUONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Yohana 14:16-31

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 14:16-31

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" (Yohana 15:7).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu jinsi ya kuongozwa na Roho Mtakatifu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Njoo na bakuli, maji, kipande cha chuma (au msumari), na mbao fupi ya



Mungu. 4. Alitaka kupaa juu kupita vimo vya mawingu. 5. Alitaka kufanana na Mungu aliye juu.

Habari za mwanzo na kuanguka kwa Shetani ni za kusisimua sana kufundisha. Unaweza kutumia mifano mingi ya maisha unapofundisha wanafunzi wako.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Uliza: "Je! mwanzo na kuanguka kwa Shetani kunatufundisha nini?" Waonyeshe maneno uliyoandika ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Utapata majibu kama: Watu huanza vizuri lakini hushindwa kumaliza. Shetani anatujaribu siku hizi tufuate mfano wake mwovu. Andika yote wanayosema. Usikubali wala kukutaa maoni yao.

Soma mafungu haya mawili, Ezekieli 28:12-18 na Isaya 14:12-14.

Uliza: "Je, mafungu haya mawili yanatufundisha nini kuhusu mwanzo na kuanguka kwa Shetani?" Wape muda wa kujadiliana.

Uliza: "Je! umewahi kumwona mtu mashuhuri ambaye ameachishwa kazi? Je! alikosa nini?" Ngojea wajibu. Wape muda wa kuongezea orodha uliyoandika.

Uliza:"Je! kutafanyika nini kama utapewa mamlaka lakini uanze kujivuna na kuwanyanyasa wenzako?" Ngojea wajibu.

**MAELEZO**

Sema: "Maandiko tuliyosoma katika Ezekieli na Isaya yanatuambia kuhusu Shetani. Ezekieli alizungumzia juu ya mfalme wa Tiro. Isaya alizungumzia juu ya mfalme wa Babeli, lakini wote wanaelezea habari za Shetani. Wanatuambia kuhusu mwanzo na kuanguka kwa Shetani.

"Ezekieli ametuambia chanzo cha Shetani. Ametuambia jinsi Shetani alivyoishi kabla ya kuanguka kwake. Shetani alikuwa mkamilifu, mwenye hekima na mzuri. Aliishi Adeni (Edeni), bustani ya Mungu. Alikuwa kiongozi wa malaika wote wa mbinguni. Hata alikuwa na malaika aliyemlinda. Lakini Je! kulitokea nini? Alipotoshwa na dhambi, hekima, uzuri, ukamilifu na cheo. Alianza kujivuna badala ya kunyenyekea mbele za Mungu. Aliadhibiwa kwa sababu ya dhambi zake. Aliteketezwa na moto. Alipoteza vyote alivyokuwa navyo.

"Isaya anatuambia kuhusu tamaa aina tano zilizomwangusha Shetani." (Andika tamaa hizo ubaoni au kwenye karatasi kubwa.)

"Alitamani 1. kuwa mkuu, 2. kuwa juu ya vyote, 3. kuwa kiongozi anayeheshimiwa, 4. kuwa juu ya viumbe vyote, 5. kuwa Mungu."

Sema: "Shetani hutujaribu tufuate mfano wake. Hutushawishi tutamani vitu ambavyo vitatuelekeza kufanya dhambi. Tunapaswa kumshinda Shetani kwa kutofanya dhambi. Kristo atatupa nguvu na uwezo wa kumshinda Shetani."

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Sema: "Shetani alianguka kutoka katika utukufu wake kwa sababu ya majivuno (kiburi). Alitumia cheo chake mbinguni kujitakia makuu. Alijaribu kujilinganisha na Mungu. Alitaka kuwa kama Mungu. Mungu alimzuia Shetani na nia yake mbaya.

"Mithali 16:18 inasema, 'Kiburi hutangulia uangamivu; Na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko.'

"Shetani alimjaribu Hawa katika bustani ya Edeni. Katika Mwanzo 3:5 alimwambia Hawa kwamba atakuwa kama Mungu



"Wafilipi 2:5-8 inatuambia mengi jinsi Yesu alivyojinyenyekeza na kuacha mamlaka yake mbinguni, ili awe mtumwa na afe msalabani. Yesu alivua utukufu wake ili amwokoe mwanadamu mwenye dhambi." (Tazama sehemu ya Msingi wa Somo Hili.)

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Sema: "Yesu ni mfano wetu jinsi ya kuishi kwa unyenyekevu. Hakufikiria ukuu wake. Alitoa maisha yake kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi. Hapakuwa na dhamana kuu ya kulipa zaidi ya hii. Wala hakuhesabu gharama.

"Yesu alijua kwamba hakukuwa na njia nyingine ambayo mwanadamu angeokolewa. Alitupenda kiasi kwamba aliamua kutufia. Wajibu wetu ni kukubali kifo na kufufuka kwake kwa ajili ya dhambi zetu. Ni lazima kila mmoja akubali hivyo."

Uliza: "Je! tunaweza kujifunza nini kuhusu uvumilivu wa Yesu? Amesema, 'Kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa naye ajidhiliye atakwezwa' (Luka 14:11)."

Uliza: "Je! mtu anawezaje kujinyenyekeza?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema: "Hapaswi kujikuza mwenyewe. Anastahili kuwafikiria watu wengine na mahitaji yao kuwa muhimu kuliko yake mwenyewe."

Uliza: "Je! mtu anapaswa kujikana mambo yapi?" Pengine wanafunzi watajibu. Wape muda wa kutoa maoni yao.

Sema: "Mtu anaweza kuacha uchoyo na ulafi. Pia anaweza kuacha matendo maovu kama makundi mabaya, kulewa, kuivuta sigara, uzinzi na uvivu. Badala ya kufanya mambo haya unaweza kijizoesha kuomba, kusoma Biblia na kushuhudia.

## MAELEZO

Mwalimu, tumia maelezo ya Msingi wa Somo Hili kwa kuwaelezea wanafunzi vifungu hivi. Waambie pia wafungue katika Luka 1:26-2, lakini hutakuwa na wakati wa kusoma sura hizo. Vifungu hivi vinaelezea kazi ya Roho Mtakatifu wakati wa kuzaliwa kwa Yesu.

Sema: "Yohana 1:1 inatuonyesha kwamba Yesu alikuwa pamoja na Mungu Baba tangu mwanzo. Alikuwepo wakati wa uumbaji. Mwanzo 1:26 inasema, "Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;....'

Uliza: "Je! unafikiri alikuwa akimwambia nani?" Wape muda wa kujibu.

Sema: "Mungu alikuwa akimwambia Yesu na Roho Mtakatifu. Wote walikuwepo na wakashiriki katika uumbaji. Tafadhali mmoja wenu asome Yohana 1:3.

"Yohana 1:1 inatuonyesha cheo cha Yesu kabla ya kuja ulimwenguni. Alikuwa pamoja na Mungu, na alikuwa Mungu. Alikuwa na haki na uwezo wa Mungu, lakini alikuwa tayari kuacha vyote na kuja ulimwenguni kama mwanadamu. Alikuja ili afie dhambi za wanadamu ndipo wapate uzima wa milele pamoja na Baba.

"Kifungu cha 10 kinaeleza kwamba watu wengi hawakumtambua Yesu. Hawakutaka nuru iwepo ulimwenguni kwa sababu walipendelea kukaa gizani ili maovu yao yasionekane. Hata watu wa kwao, Wayahudi, hawakumkaribisha. Soma kifungu cha 11.

"Vifungu vya 12-14 vinaonyesha baraka kuu ambazo wangepewa wale watakaomwamini. Walipokea uwezo wa kufanyika wana wa Mungu.



akiwa atakula tunda la ujuzi wa mema na mabaya. Hawa alifanya dhambi kwa sababu alimsikiliza.

"Shetani angali anatujaribu hata sasa. Anataka hasa kutufanya wake. Hutumia njia nyingi kutufanya tumwamini. Hutumia elimu yetu, kazi, mali na hata marafiki kutufanya tushuku imani yetu katika Kristo. Hutumia wajibu wetu kanisani na kwa jamii kutujaribu. Hutufanya tutumie lugha chafu, tusikilize muziki mbaya na kusengenyana. Lakini wote wanaomwamini Shetani huanguka.

"Warumi 12:21 inasema, 'Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema?' Ni rahisi kwetu kuvutwa na maovu, lakini tunaweza kushinda maovu kwa kujificha katika Kristo Yesu. Yesu ndiye mfano wetu. Anataka tufanye mema badala ya kusema maneno matupu. Anataka tuwe wapole kwa wenzetu, hata adui zetu. Anataka tuwe wakamilifu mbele za Mungu. Anataka tutafute hekima ya Mungu badala ya kutegemea hekima yetu wenyewe. Tutamshinda Shetani kama Kristo anaishi ndani yetu."

## KUOMBA

1. Waombee wanafunzi wako waweze kuelewa mwanzo na kuanguka kwa Shetani. Waombee watambue kwamba yeye ni hatari maishani mwao.

2. Waombee wanafunzi wako waweze kumshida Shetani na majaribu yake.

3. Mwombe Roho Mtakatifu akuongoze unapofudisha somo hili.

## SURA YA PILI

# SHETANI, KAZI YAKE SIKU HIZI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Zakaria 3:1; Mwanzo 3:1-7; Ayubu 1:9; Mathayo 13:19; 4:3; Luka 11:14-26

VIFUNGU VYA LEO: Zakaria 3:1; Mwanzo 3:1-7; Ayubu 1:9; Mathayo 13:19; 4:3; Luka 11:14-26

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze" (1 Petro 5:8).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kazi anayofanya Shetani siku hizi.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Andika maneno haya ubaoni au kwenye karatasi kubwa: Kazi ya Shetani Leo.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Shetani anafanya kazi kwa bidii kwa sababu anajua kwamba kazi na utawala wake unakaribia kwisha. Muda wake ni mfupi sana. Anamwogopa Mungu kwa sababu ya uwezo na hekima yake.

Shetani angali anafanya kazi hata sasa. Hajaacha kamwe ingawa amefungwa na Kristo. Bado anafanya kazi aliyoianza wakati wa kuanguka kwake. Bado anatumia hata sasa vishawishi alivyotumia kujaribu Hawa, Ayubu na Yesu.

Katika Zakaria 3 na Ayubu 1:9, 2:4, Shetani alitumia hila ya kushitaki. Je! kwa nini Shetani alishitaki taifa la Israeli (Yoshua) na Ayubu mbele za Mungu?



Kwanza, Paulo anatukumbusha kwamba Yesu alikuwa namna ya Mungu. Neno hili la Kiyunani, namna, linamaanisha kwamba kitu kisichobadilika kamwe. Yesu alipofanyika mwili hakubadili asili yake ya Mungu. Alikuwa Mungu hata baada ya kufanyika mwili. Mungu Baba na Yesu Kristo walikuwa namna moja katika utu na umbo, na walikuwa cheo sawa.

Pili, anatuambia katika kifungu cha 7 na 8 kwamba alijiondolea ule usawa na Baba. Alibaki mwenye umbo sawa na Mungu, lakini akaacha uwezo wake. Yesu alipofanyika mwili, aliacha utukufu wake na kujinyenyekeza akatwaa namna ya mtumwa. Hata alikubali kuwa sadaka iliyotolewa msalabani. Alikuwa mfano wa mwanadamu na kubakia na umbo la Mungu.

Mwishowe, Paulo anatuambia katika vifungu vya 9-11 kwamba Mungu alimtukuza Yesu Kristo. Kwanza, Mungu alimpa jina lililopita kila jina. Pili jina lake lingetambuliwa na kila mtu. Yesu akasema, "Kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa" (Luka 14:11).

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Unaweza kuwasaidia wanafunzi waelewe namna mbili ya Mungu kwa kuwaonyesha shilingi. Utaona kwamba shilingi ina pande mbili ambazo haziwezi kutengeanishwa. Sehemu hizi mbili ni tofauti. Uliza kwamba shilingi hiyo inawezwa kutumiwa kama shilingi mbili kwa sababu ina sehemu mbili tofauti. Yesu ana umbo aina mbili kama shilingi hii.

Waambie wanafunzi wafungue Yohana 1:1-14 na wasikilize mmoja wao akisoma

## MSINGI WA SOMO HILI

Yesu alikuwa na utu aina mbili usioweza kutenganishwa: alikuwa Mungu na Mwanadamu. Je! alipataje utu huu?

Luka 1:34-35 inasema, "Mariamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijui mume? Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu." Roho Mtakatifu alihusika katika kufanyika kwa Yesu kuwa mwanadamu.

Yohana 1:14 inatuambia kwamba Neno lilikuwepo hata kabla ya kuuumba ulimwengu. Neno lilikuwepo wakati ulimwengu ulipoanza. Neno ambalo Yohana anatuambia katika kifungu cha 14, ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Vitu vyote viliumbwa kupitia kwake. Yeye ndiye chanzo cha nuru na uzima.

Pili, Yohana anasema, "...naye Neno alikuwako kwa Mungu..." (Yohana 1:1). Yohana anatuambia kuhusu uhusiano ulioko kati ya Neno la Mungu. Uhusiano huu unaweza tu kuelezwa na maneno yake mwenyewe. Walikuwepo pamoja "hapo mwanzo."

Tatu, Yohana anasema, "...naye Neno alikuwa Mungu." Hasemi kwamba Neno alikuwa kama Mungu. Neno ni Mungu. Yesu Kristo ndiye Neno hilo. Tunapomwona Yesu huwa tunamwona Mungu kwa mawazo, moyo, muumba na umoja.

Soma pia Luka 1 na 2 kujua jinsi Neno lilivyofanyika mwili. Utaona jinsi Roho Mtakatifu alivyohusika katika tendo hilo.

Sasa soma Wafilipi 2:5-11. Paulo alituandikia mfano jinsi ya kuwa wapole. Yesu Kristo ndiye mfano wetu wa uvumilivu.



Kwanza, Shetani alilionea taifa la Israeli na Ayubu wivu, uchungu na chuki. Aliwachukia kwa sababu Mungu aliwapenda. Shetani huwashitaki waliookoka siku hizi kwa kutumia sababu hiyo hiyo. (Ufunuo 12:10)

Mwanzo 3:1-7 inatwambia kwamba ni mdanganyi. Tunaambiwa kwamba alimdanganya Hawa na kumfanya ashuku Neno la Mungu. Shetani siku hizi anaudanganya ulimwengu wote. (Ufunuo 12:9)

Tunaambiwa katika Mathayo 4:3 kwamba Shetani hujaribu watu. Anataka kuwaangusha watu. Shetani alimjaribu Yesu, na bado atatujaribu. (1 Wakorintho 10:13) Si dhambi kujaribiwa, lakini huwa dhambi tunapoanguka majaribuni. Soma Waebrania 4:15. Yesu alijaribiwa lakini hakufanya dhambi. Hatupaswi kushikilia dhambi zetu tunapoanguka majaribuni. Tunapaswa kukiri mbele za Mungu. (1 Yohana 1:9)

Mathayo 13:19 inatuambia kwamba Shetani anataka kuharibu kila kitu. Anaitwa mwovu. Nia yake ni kukifanya kila kitu kuwa kiovu. Hutaka kuona kwamba watu wanafurahia maovu, kwa mfano, vita, uongo, wizi, uhalifu na kudanganya. Yesu alituombea tusije tukapatwa na nguvu za Shetani (Yohana 17:15) ambazo zinauzunguka ulimwengu wote. (1 Yohana 5:19)

Shetani ameitwa Beelzebul katika Luka 11:14-26. Jina hili linamwonyesha Shetani kuwa ni mtawala. Anataka kutawala maisha ya watu. Huwaamuru watu wafuate mfano wake mbaya wa kufanya maovu. Watu wengi humtii Shetani bila kujua wanalofanya. Wanahitaji kusaidiwa.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Uliza: Je! Shetani hufanya kazi gani siku hizi?" Waonyeshe maneno uliyoandika ubaoni, au kwenye karatasi kubwa.

Sema: "Hebu tutafute jibu la swali hili katika Biblia." Waambie wasome Maandiko ya Biblia ya somo la leo. Watapaswa kuinua mikono na kujibu wanapoona kitu cho chote ambacho Shetani anafanya. Andika majibu yao ubaoni.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Utangulizi ulioko katika kitabu cha wanafunzi.

Uliza: "Je! mbwa aliyefungwa huwabwekea watu? Je! watu humwopa? Je! huacha kubweka kwa sababu amefungwa?" Ngojea wajibu kila swali, kisha uliza: "Kwa nini?" Linganisha mfano huu na kazi ya Shetani. Wasaidie wanafunzi wafahamu kwamba matokeo ya kazi ya Shetani yameshindwa na Kristo. Sisi Wakristo tuko huru. Hatuko watumwa wa Shetani. (Waebrania 2:14-15)

**MAELEZO**

Sema: "Vifungu vyote tulivyosoma vinazungumzia juu ya kazi ya Shetani. Hushawishi kupitia kwa kazi yake. Ni lazima tufahamu kwamba Shetani alikuwepo hapo zamani. Bado anafanya kazi hata sasa. Tunapaswa kumshida kwa kujifunza na kutambua jinsi anavyowashawishi Wakristo."

Sema:"Malaika alimwonyesha Yoshua kwa Zakaria katika Zakaria 3:1. Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu. Yoshua aliiwakilisha Yerusalemu au wateule wa Mungu. (kifungu cha 2) Yoshua, au wateule wa Mungu, walisimama mbele za Mungu katika nguo chafu (dhambi). Shetani naye alisimama katika mkono wa kuume wa Yoshua na kumshitaki. Tunaambiwa kwamba Mungu alimkemea Shetani. Shetani



**KUOMBA.**

1. Omba kwamba wanafunzi wako wataelewa maana ya kujazwa na Roho. Omba kwamba watarekebisha nia yo yote mbaya waliyonayo.

2. Waombee wanafunzi wako wajazwe Roho Mtakatifu unapoendelea kuwafundisha.

3. Waombee waone kuwepo kwa ushahidi wa Roho maishani mwao.

4. Mwombe Roho Mtakatifu akutumie unapowafundisha.

## SURA YA KUMI NA MBILI

# ROHO ALIFANYIKA MWILI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Luka 2; Yohana 1:1-14; Wafilipi 2:5-11

VIFUNGU VYA LEO: Luka 2; Yohana 1:1-14; Wafilipi 2:5-11

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake..." (Yohana 1:14).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Yesu Kristo ni Mungu, lakini alikuja duniani kama mwanadamu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Andika maneno haya kwenye ubao au karatasi kubwa: Yesu Kristo, Mungu na Mwanadamu.

Sema: "Fungu la Wagalatia linatufundisha kuhusu mojawapo ya ushahidi wa Mkristo aliyejazwa Roho Mtakatifu. Nao ni tunda la Roho." Eleza pia ushahidi mwingine kutoka Msingi wa Somo Hili.

Sema: "Hebu tusome Waefeso 4:25-32. Fungu hili linatuonyesha jinsi mtu anavyostahili kuwa baada ya kujazwa Roho Mtakatifu. Soma pia Waefeso 5:18.

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Uliza: "Je! unajua mtu ye yote ambaye amejazwa Roho Mtakatifu? Je! ilifanyikaje hivyo? Je! wewe umejazwa Roho Mtakatifu?" Endelea bila kungonjea wajibu.

Uliza: "Je! unawezaje kujua kwamba wewe mwenyewe au mtu mwingine amejazwa Roho Mtakatifu?" Wape muda wa kujadiliana.

Hiki ndicho Kifungu cha Kukumbuka cha leo, kwa hiyo mkisema pamoja mpaka watakapokijua kabisa. Waelezee kwamba kuomba inamaanisha kumtegemea Mungu. Kutafuta inamaanisha ni lazima wachukue wajibu, kwa mfano, kuomba, kusoma Biblia zao, na kumwamini Mungu. Kubisha inamaanisha waendelee kumtegemea Mungu na wafanye mambo anayowaongoza kufanya. Wahakikishie wanafunzi kwamba kila Mkristo ana Roho Mtakatifu. Hawangeokolewa bila ya Roho Mtakatifu. Wanapaswa kufurahia kujazwa mara nyingi ili wawe mashahidi wema wa Yesu Kristo.

Uliza: "Je! kwa nini ni muhimu kwa Mkristo kujazwa Roho Mtakatifu?" Waambie wasome Wagalatia 5:22-23 kama msaada wa kujibu swali hili.



alinyamazishwa. Je! kwa nini Mungu alimnyamazisha Shetani? Mungu alimchagua Yoshua hataingawa alikuwa mwenye dhambi. Ilikuwa kazi ya Mungu kumwokoa kutoka dhambini. Shetani hakuwa na haki ya kumshitaki.

"Tunasoma katika Mwanzo 3:1-7 kwamba Shetani alimdanyanya Hawa. Nyoka alikuwa mnyama wa mwituni ambaye Shetani alimtumia kumdanganya Hawa. Jaribu lilianza wakati nyoka alipomdanganya Hawa kushuku Neno la Mungu.

"Vifungu vya 1-3 kinasema, '...Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu...?' Nyoka alimshawishi Hawa ashuku nia ya Mungu. Vifungu vya 4 na 5, '...Hakika hamtakufa...mtafumbuliwa macho....' Hawa alikula tunda hilo, akafumbuliwa macho kuona dhambi. Alianza kujua mema na mabaya. Yeye na Adamu walitambua kwamba wako uchi. Walianza kuhofia kuvunjika kwa ushirika wao na Mungu. (Vifungu vya 8-13) Walitambua kwamba Mungu ni mtakatifu, nao ni wenye dhambi. Shetani bado hutudanganya siku hizi.

"Mathayo 4:3 inatuambia kwamba Shetani hutujaribu. Shetani alitaka kumfanya Yesu ashuku kwamba yeye ni Mwana wa Mungu! '...Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu...,' akamwambia. Shetani alitaka Yesu aanguke, lakini Yesu alimshida kwa kutumia Neno la Mungu. Yesu alimjaribu kila wakati kwa kusema, 'Imeandikwa...'"

Sema: "Tunasoma katika Mathayo 13:19 kwamba Shetani ni mwovu. Yesu alimwita Shetani mwovu. Yesu anasema kwamba kazi ya Shetani ni kunyakua Neno la Mungu kutoka kwa watu. Watu waovu wanapokosa Neno la Mungu. Shetani hujishughulisha siku hizi kuhakikisha kwamba watu hawana Neno la Mungu mioyoni mwao. Shetani anajua kwamba mwanadamu atakuwa mwovu kama hana Neno la Mungu mwoyoni mwake.

"Tunasoma katika Luka 11:14-26 kwamba Shetani ni mtawala. Hii ndiyo maana ya jina hili Beelzebuli. Shetani ni mtawala. Hutawala mawazo, moyo na mwili mtu ambaye hajaokoka. Huwafanya watu wawawazie maovu wengine, wasengenye na kutendeana maovu."

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Uliza: "Je! Shetani bado anafanya kazi siku hizi? Ndiyo! Angali anawadanganya na kuwajaribu watu. Anawawinda sana hasa Wakristo. Hajishughulishi na wale ambao si Wakristo. Wao ni wake.

"Je! tunawezaje kujilinda kutoka kwa mishale ya mwovu Shetani? (Waefeso 6:16) Ni lazima tumtegemee Bwana ambaye ni ngao na nguvu zetu. Atatupa neema yake na uwezo wa kumshinda Shetani kama tutamtafuta yeye na njia yake."

Uliza: "Je! unawezaje kumpinga Shetani?" Wape muda wa kujadiliana. Kisha waambie wasome 1 Petro 5:8. "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye...."

Sema: "Kifungu hiki kinatukumbusha kwamba Shetani atatufanyia hila. Tumeambiwa tukeshe na kujihadhari ili tusianguke Shetani ajapo.

"Tunapaswa pia kumpinga kwa kutumia Neno la Mungu. Hatatujia tuwapo na Neno la Mungu mioyoni mwetu."

Uliza: "Je! umekariri vifungu vingapi ili uvitumie kumpinga Shetani anapokujia?

Endelea: "Hatupaswi kuupenda ulimwengu au vitu vilivyomo ulimwenguni. Shetani hututega kwa kutumia vitu tunavyopenda. Hutufanya tutamani vitu ambavyo havidumu. Hutujaza tamaa ya mwili na tamaa ya macho.



Ushahidi wa pili ni ujasiri wa kuhubiri injili ya Yesu Kristo. Soma 2 Timotheo 1:7 na Matendo 9:27-29. Mungu atatupa ujasiri.

Ushahidi wa tatu ni utumiaji mzuri wa karama za kiroho. Soma Matendo 2:4 na 1 Wakorintho 12:30-31. Wakristo hupewa karama na Roho Mtakatifu wazitumie katika huduma ya Kikristo. Lengo lake ni kuwasaidia wengine wakue kiroho na wamtukuze Mungu. Hawapewi kwa manufaa au sifa za mtu binafsi.

Tunaweza kusema kwamba Mkristo huendela kujazwa Roho Mtakatifu.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Uliza: "Je! nini maana ya kujazwa na Roho Mtakatifu? Waonyeshe maneno uliyoandika ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Pengine watakujibu: Wakati tunda la Roho linapoonekana kwa ujasiri na uwezo, au wakati mtu anapotumia vizuri karama za kiroho. Andika majibu yao na usikubali wala kukataa lo lote.

Wachague wanafunzi wawili wasome Maandiko ya leo. Wanafunzi wengine wajaribu kutafuta mafundisho ya kila fungu. Kisha waseme mafundisho sahihi kutoka katika ordha uliyoandika. Ongeza mafundisho hayo.

**MAELEZO**

Sema: "Mafungu tuliyosoma katika Injili ya Yohana na Wagalatia yanatufundisha kuhusu kujazwa Roho Mtakatifu. Fungu la Injili ya Yohana linatufundisha kuhusu masharti ya kujazwa Roho Mtakatifu." Mwalimu, waelezee wanafunzi masharti haya ukitumia maelezo ya Msingi wa Somo Hili.

Sharti la kwanza ni kuona kiu. Yaani Mkristo anapaswa kuwa na hamu ya kujazwa. Yesu alizungumzia kuhusu kiu ya kiroho. Mtu anapoona kiu ya maji, yeye hunywa maji. Lakini hitaji la kimwili haliwezi kutosheleza kiu ya kiroho. Mtu awapo na kiu ya kiroho huhitaji chemchemi ya maji ya Kiroho kububujika maishani mwake. Huyo ndiye Roho Mtakatifu.

Sharti la pili ni kumwendea Yesu. Mtu anapokuwa na kiu huenda kwenye mtungi au bomba kuchota maji. Vivyo hivyo ni lazima mtu amwendee Yesu awapo na kiu ya kiroho. Je! inamaanisha nini kumwendea Yesu? Inamaanisha useme naye, ujitoe kwake na umtegemee yeye. Yesu ni Mwokozi wetu.

Mkristo humwendea Yesu kwa moyo na nia ya upole na kumwambia mahitaji na shida zake zote. Hitaji mojawapo la Mkristo ni kumwomba Yesu amjaze Roho Mtakatifu. Yesu atampa kila anachohitaji.

Sharti la tatu ni kunywa. Mtu aliye na kiu apatapo maji huanza kunywa. Mtu aliye na kiu ya kiroho amjiapo Yesu kwa maombi, huanza kunywa kiroho. Husoma Neno la Mungu na kulitafakari. Hujiunga na watu wengine kwa ibada na kujifunza Biblia. Atatoshelezwa anapoendelea kunywa.

Sharti la nne ni kuamini. Mtu anapojua ana kiu, humwomba Mungu na huanza kunywa Neno la Mungu. Anapaswa kuamini kwamba yuko mbele za Mungu. Ni lazima aamini kwamba anajazwa na Roho Mtakatifu. Ni lazima awe na imani kwa sababu imani humpendeza Mungu. Atajazwa Roho Mtakatifu kwa kumwamini Mungu.

Kuna ushahidi aina tatu wa kumsaidia Mkristo kufahamu kwamba amejazwa Roho Mtakatifu.

Ushahidi wa kwanza ni tunda la Roho. "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi;..."(Wagalatia 5:22- 23).



"Shetani hutaka kuharibu ushirika wetu na Mungu. Wakristo wanapaswa kufurahi katika Bwana kwa sababu Kristo ameshinda vita. Soma 1 Yohana 4:4 na ukitumie unapojaribiwa na Shetani."

**MAOMBI**

1. Waombee wanafunzi wako waweze kuona na kutambua hila za Shetani maishani mwao.

2. Waombee waweze kusimama imara na watumie Neno la Mungu kumpinga Shetani.

3. Waombee wanafunzi wako wajizoeshe kujifunza Biblia ili wajue Neno na ahadi za Mungu na kuzitumia.

4. Mwombe Mungu akujaze Roho Mtakatifu wewe na wanafunzi wako. Mwombe atawale maisha yenu.

## SURA YA TATU

# SHETANI NA HUKUMU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Ufunuo 19:11-21; 20:1-9; Ayubu 1:6-12; Mathayo 25:41

VIFUNGU VYA LEO: Ufunuo 20:1-9

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "...Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba hawapaswi kuogopa majaribu ya Shetani kwa sababu kazi na uwezo wake utashindwa siku ya hukumu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki au karatasi kubwa. Andika swali hili: Je! Shetani ni nani?

**MSINGI WA SOMO HILI**

Somo hili linatoka katika kitabu cha Ufunuo. Utagundua unapoendelea kujifunza kwa nini Mungu anamruhusu Shetani kuendelea kuwavamia watu na kanisa. Utajifunza pia kwamba Mungu atakuja kumwangamiza Shetani.

Kitabu cha Ufunuo ni cha unabii. Mtume Yohana ndiye mwandishi. Inakisiwa kiliandikwa mwaka wa A.D. 96. Mafundisho ya kitabu hiki yanahusu kupingana kwa roho. Kiliandikiwa Wakristo walioteswa wa karne ya kwanza. Walishuku kama Ukristo utakuja shinda nguvu za Shetani.

Ufunuo 19:11 inatupa picha ya siku hiyo inayokuja. Mfalme wa waaminifu na hakimu wa haki watapigana vita. Mwana wa Mungu hatawahurumia wapotevu. Mtu anapokuwa Mkristo, huwa mfuasi wa Yesu. Mtu huyu atapata uzima wa milele.

Kifungu cha 12: Kuna uwezo mkuu ambao utapigana vita vya mwisho na Shetani. Mwenendo mwovu wa Shetani utakujaisha siku hiyo. Tunapaswa kutii amri za Mungu. Imani yetu katika Kristo inapaswa kuwa imara, isiyotikisika.

Kifungu cha 13: Damu ya Yesu imesafisha dhambi zetu. Tunapaswa kutambua kwamba damu ya Yesu ni ya muhimu sana kwa Mkristo.

Vifungu vya 15-21: Tunamwona Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana aliyepigana na kazi ya Shetani na kumshinda. Anawaita ndege wote waje na kufurahia chakula cha Mungu. Watakula nyama ya watu walioanguka, wadogo kwa wakubwa. Tunapaswa kufahamu kwamba ahadi ya Mungu ni ya kweli, hukumu inakuja.



**SURA YA KUMI NA MOJA**

## KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Yohana 7:37-39; Wagalatia 5:22-23

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 7:37-39; Wagalatia 5:22-23

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa" (Mathayo 7:7).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafunza wanafunzi wangu maana ya kujazwa Roho Mtakatifu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Andika maneno haya ubaoni au kwenye karatasi kubwa: KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Je! inamaanisha nini kujazwa na Roho? Je! jambo hili hufanyikaje? Je! ni nini ishara ya mtu aliyejazwa Roho? Petro anatuambia, "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho" (Waefeso 5:18). Je! alimaanisha nini?

Paulo alimaanisha kwamba Mkristo anapaswa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Maisha yanayoongozwa na Roho Mtakatifu huonesha upendo, amani, furaha, upole, uvumilivu na wema. Mkristo hapaswi kamwe kuongozwa au kutawaliwa na tamaa za mwili au Shetani. Yeye anayeongozwa na tamaa za mwili huwa na hasira, chuki, mwizi, mwongo na mzinzi.

Je! Mkristo anawezaje kujazwa na Roho? Soma Yohana 7:37-39. Kuna masharti manne katika fungu hili ya kutimiza ndipo Mkristo ajazwe na Roho.

akampeleka mbinguni kabla ya kufa, alipomaliza kazi yake duniani.

"Roho anaishi ndani yako kama umemwamini Yesu Kristo. Huja kuishi milele unapompokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wako. Huongoza uamuzi wako na hukusaidia kuelewa mapenzi ya Mungu maishani mwako.

"Roho hukupa amani na uzima, lakini ulimwengu utajaribu kukuzuia kufuata uogozi wa Roho maishani mwako. Usivutiwe na mambo ya ulimwengu. (Warumi 12:2) Kubali na upokee uwezo wa Yesu kukusaidia kushinda ulimwengu.

"Wewe kama Mkristo, mwamini unapaswa kutembea kama Kristo. Kristo ndiye mfano wetu wa kufanya mapenzi ya Baba. Tuanze kutembea pamoja na Mungu jinsi Roho anavyotuongoza."

Uliza: "Je! utamruhusu afanye kazi ndani yako na akutumie leo? Je! uko tayari kumwacha Roho atawale maisha yako? Je! umeona jinsi tunavyopaswa kutembea na Roho?"

Sema: "Roho Mtakatifu hutimiza yote ambayo Mungu hutaka. Ndiye ahadi ya Mungu ya uzima ulikuja na Yesu Kristo. Yesu atakujaza na Roho wake kama utamwambia, ndiyo Bwana. Atakaa na kufanya kazi maishani mwako milele."

## KUOMBA

1. Waombee wanafunzi wako waelewe kazi ya Roho Mtakatifu siku hizi.

2. Omba kwamba watamwomba atawale maisha yao.

3. Waombee wale ambao wanahudhuria masomo ya Biblia lakini hawajaokoka.



Tunaona katika kitabu cha Ayubu kwamba Mungu alimruhusu Shetani amjaribu Ayubu, lakini imani yake ilikuwa imara. Shetani alishindwa. Mungu hamwogopi Shetani. (Yohana 16:1)

Tunapaswa kuamua sasa ili tusitupwe katika ziwa la moto. Mathayo 25:41 inasema, "Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake."

## KULIFUNDISHA SOMO

## UTANGULIZI

Uliza: "Je! Shetani ni nani?" Waonyeshe swali hili uliloandika ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Andika ubaoni majibu yao. Wanaweza kujibu kwamba ni roho mchafu, yule anaye wajaribu watu au ni adui wa Wakristo. Wanafunzi wanaweza kuangalia pia majibu ya swali hili katika sura ya kwanza na ya pili (kitabu hiki). Baada ya kumaliza kujibu, soma Ufunuo 19:11-21.

Sema: "Tunaona katika vifungu hivi jinsi kazi ya Shetani itakavyotupwa katika ziwa la moto." Waulize wanafunzi waseme baadhi ya kazi anayofanya Shetani siku hizi. Tena, wanaweza kupata majibu zaidi katika masomo waliyojifunza.

Sema: "Shetani alitupwa nchini kutoka mbinguni. Anaishi pamoja nasi. Anajaribu kumtafuta mtu wa kumeza kwa kuzunguka-zunguka kama simba anayenguruma." Soma Zakaria 3:1 na 1 Petro 5:8.

Soma Ufunuo 20:10. Sema: "Ibilisi atatupwa Jehanum. Jehanum haikutengenezwa mwanadamu. Ilitengenezewa Ibilisi na malaika zake. Mwanadamu ataenda Jehanum kwa sababu anamtii Shetani badala ya kumwamini Yesu Kristo."

## MAELEZO

Sema: "Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa mwaka wa A.D. 96 na mtume Yohana. Kitabu hiki kiliandikiwa Wakristo walioteswa wa karne ya kwanza. Walikaribia kufa moyo iwapo Ukristo utashinda nguvu za Shetani.

"Kitabu hiki kinatwambia kwamba Shetani ameshindwa, nao wako katika ushindi huo. Mungu anazungumzia kuhusu hukumu ya Magedo. Kristo ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Kristo ana uwezo juu ya viumbe vyote. Tunapaswa kujua kwamba yeye pekee ndiye mwenye uwezo. Jeshi la mbinguni linatuonyesha malaika na watakatifu wa mbinguni.

"Mwandishi ameonyesha mwisho wa Shetani. Tunaona kwamba adui huyu na manabii wa uongo watateseka milele na milele. (Ufunuo 20:10) Mungu anataka tuchague wa kufuata, Kristo au Shetani."

## UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Uliza: "Je! ni nani aliyeumba Shetani?" Wape muda wa kujibu.

Uliza: "Je! kwa nini Mungu anamruhusu Shetani aendelee kumpinga yeye na watu wake?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema: "Shetani hakuwa akitawala jeshi lake kabisa alipofukuzwa kutoka mbiguni. Alihitaji wakati wa kutumia hila zake. Shetani anafikiri kwamba anaweza kumshinda Mungu. Mungu amempa Shetani nafasi ya kutayarisha jeshi lake la kupigana vita vya mwisho. Shetani anamini kwamba atashinda, lakini ufunuo unatuambia kwamba Mungu atashinda naye Shetani ataangamizwa."

Uliza: "Je! Mungu huwajaribu watu wake?" (La, hasha! Mungu hamjaribu mtu ye yote, lakini humruhusu Shetani atujaribu.)



katika maisha ya Yesu. Tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu Mwana na Mungu Roho ni mmoja."

Uliza: "Je! Roho hufanya kazi gani katika mwamini?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema: "Roho Mtakatifu huwavuta watu kwa Yesu Kristo kwa kuwaonyesha dhambi zao. Huwaonyesha uovu wao na huwasaidia wanapozaliwa upya katika jamaa ya Mungu. Hatimaye Roho huishi ndani ya mwamini na huenenda naye kama msaidizi mfariji na rafiki.

"Tunaweza kuwa washindi na wajasiri kama tutafuata uongozi wa Roho, lakini tutashindwa kama tutadai kutawala maisha yetu. Kila mwamini awapo dhaifu au mwovu, anaye Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu humwunganisha mwamini na Mungu. Uwepo na Roho huonyesha utawala wa Mungu. Sisi tu mali ya Mungu kwa sababu tumenunuliwa na damu ya Yesu.

"Roho hutenga wa ulimwengu na hutufanya tumtukie Mungu. Hutuongoza kufanya mapenzi ya Mungu."

## UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Roho Mtakatifu anauwezo juu ya ulimwengu wote. Yeye ni sawa na Mungu Baba na Mwana, Yesu Kristo. Ametuachia tuamue kiwango ambacho tunataka atawale maisha yetu. Hatatulazimisha tuokoke wala tukubali uongozi wake. Uamuzi ni wetu."

Sema: "Maisha yaliyojaa Roho ni maisha yanayoongozwa na Kristo. Huwa tunaiendelea njia ya mauti tunapojitegemea sisi wenyewe na kuishi maisha ya kidunia. Ni lazima tufanye mapenzi ya Mungu. Mfano wa mtu aliyeongozwa na Roho ni Enoko. Enoko alitembea na Mungu mwishowe Mungu

Luka 1:35; Mathayo 3:13-17; Yohana 14:16- 20; Warumi 8:6-14.

Uliza: "Je! tunajifunza nini katika vifungu hivi kuhusu Roho Mtakatifu?" (Tunajifunza kwamba Mtoto wa Mariamu aliletwa na Roho Mtakatifu. Roho alifanya kazi katika maisha na huduma ya Yesu. Huwasaidia Wakristo kushiriki na Mungu. Huwaongoza waamini kufanya mapenzi ya Mungu.)

**MAELEZO**

Sema: "Roho Mtakatifu amekuwepo tangu ulimwengu ulipoumbwa. Alishiriki katika uumbaji. Mtendo na kazi ya Agano la kale yaliongozwa na Roho Mtakatifu.

"Watu wa Agano la Kale waliongozwa na Roho Mtakatifu. Aliwaongoza kutambua mwito wa Mungu kwa maisha yao. Roho aliwateua watu wa kumtumikia Mungu. Aliwapa nguvu walipofuata uongozi wake. Roho Mtakatifu aliwasaidia watu kama Ibrahimu, Musa, Eliya, Gideoni, Daudi na wengine wengi kuwa wajasiri. Walifanya maajabu kwa sababu walimtegemea Roho Mtakatifu."

Uliza: "Je! ni nini kazi ya Roho Mtakatifu katika Agano Jipya?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema: "Sehemu muhimu ya kazi yake ilianza wakati alipotabiri kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ndiye aliyetimiza kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, kupitia kwa Mariamu. Roho Mtakatifu alidhihirisha mwanzo wa huduma ya Yesu wakati alipobatizwa. (Mathayo 3:13-17) Alimsaidia Yesu kwa miujiza aliyofanya. Alimwezesha kuendeleza huduma yake. Alimsaidia wakati alipojaribiwa nyikani. Roho Mtakatifu alimfufua Yesu katika wafu.

"Maneno na kazi zote za Yesu ziliongozwa na Roho Mtakatifu. Hakuna mtu awezaye kushuku uwepo na uwezo wa Roho



Uliza: "Je! seremala anawezaje kujua kwamba kiti alichotengeneza kitadumu?" Tarajia majibu kama, atakikalia au atakitikisa.

Sema: "Mungu anataka kujaribu utii na imani ya mwanadamu. Humruhusu Shetani amjaribu mwanadamu, lakini Shetani hawezi kutujaribu kupita uwezo wetu. Mungu atatusaidia kumshinda Shetani kama tu waaminifu.

"Tunasoma katika Ayubu kuhusu mtumishi mwaminifu wa Mungu ambaye alijaribiwa. Ayubu alikuwa mtu mwaminifu. Alimcha Mungu. Shetani alifikiri kwamba Ayubu alimtii Mungu kwa sababu ya utajiri wake. Alifikiri kwamba Ayubu atamwasi Mungu kama atapoteza utajiri wake. Mungu alimruhusu Shetani amjaribu Ayubu, lakini alikuwa mwenye imani kuu. Alipoteza mali yake yote, lakini hakukana imani yake kwa Mungu. Ni lazima nasi tuwe imara katika imani yetu.

"Siku hizi watu wengi wanaishi kama kwamba hawamwamini Kristo. Wengine hawaamini kwamba Shetani yupo. Wanapaswa kujihadhari!

"Huwa tunapenda sana kuwa katikati. Biblia inatuambia kwamba Mungu atatutapika kama tu vuguvugu. Soma Ufunuo 3:15-16. Tunapaswa kuwa wa Kristo. Kama mtu hajamwamini Kristo, yeye ni wa Shetani. Shetani na wafuasi wake wametengewa ziwa la moto.

"Jehanum haikutayarishiwa mwanadamu. Ilitayarishiwa ibilisi na malaika zake. Mwanadamu ataenda jehanum kama atamtii na kumfuata Shetani badala ya kumwamini Kristo.

"Ni juu yako kuamua. Hakuna mtu atakayekuamulia. Je! utamfuata nani?"

Waamibie wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka pamoja nawe hadi watakapokisema bila kusaidiwa. Wahimize wakamilishe sehemu ya Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**KUOMBA**

1. Omba kwamba imani ya kila mwanafunzi itakua mnapojifunza masomo haya.

2. Waombee wale ambao hawajampokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao waweze kuokoka mnapojifunza masomo haya.

3. Mwombee kila mwanafunzi achague njia nzuri ya kufuata.

4. Oma kwamba kila mwanafunzi ataelewa maana ya Ufunuo 19 na 20 wanapoendelea kujifunza.

5. Mwombee kila mwanafunzi aweze kuhudhuria masomo yote ya kitabu hiki.

## SURA YA NNE

# UCHAWI NA KAZI YA SHETANI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6; Kutoka 22:18; Matendo 16:16-18; 2 Wakorintho 11:13-15

VIFUNGU VYA LEO: 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6; Kutoka 22:18; Matendo 16:16-18; 2 Wakorintho 11:13-15

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "... Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile" (Matendo 16:18).



na Mungu Roho ni mmoja. Wote hufanya kazi pamoja. Roho huwaonyesha wanadamu dhambi zao. Roho ndiye humsaidia mtu kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Roho Mtakatifu huishi ndani ya kila Mkristo. Haijalishi kama mtu ni dhaifu. Roho mtakatifu huleta ushirika kati ya mwamini na Mungu.

Yesu alipokaribia kwenda mbinguni, alimwomba Mungu Baba awaletee wanafunzi na waamini msaidizi ambaye angekuwa nao milele. Alikuwa Roho Mtakatifu. (Yohana 14:16-20) Roho Mtakatifu alimwunganisha mwamini wa Mungu. Uwepo wake katika mwamini ulionyesha kwamba yeye ni mali ya Mungu. Kuunganisha huku kwa Roho humhakikishia mwamini kwamba ameokoka.

Roho hufunuliwa kwetu kama rafiki ambaye yuko kila wakati. Hutuonyesha dhambi zetu, hutufariji na kutuelekeza kwa Mungu. Hutuonyesha maovu na ana uwezo wa kutufanya tuwe viumbe wapya. Hatuwezi kuzaliwa upya bila ya Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuwa na nguvu maishani mwetu. Wala kumpendeza Mungu bila Roho. Roho hakulazimishi kufanya mapenzi yake. Hukupa wakati wa kuamua. Ni lazima uamue kama unataka aishi ndani yako.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Sema: "Tafadhali chukueni kalamu na karatasi na mwandike majibu ya maswali haya."

Uliza: "Je! Roho Mtakatifu ni nani? Je! Roho Mtakatifu alianza lini kazi yake? Je! Roho Mtakatifu hufanya kazi gani?" Wape muda wa kuandika majibu. Kusanya karatasi hizo na uwapatie tena ili mtu asijue ana karatasi ya nani. Chagua baadhi yao wasome majibu ya karatasi walizo nazo. Kisha wachague wanafunzi wanne wasome Maandiko ya somo la leo:

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kazi ya Roho Mtakatifu maishani mwa watu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Kalamu na karatasi ya kumpa kila mwanafunzi

**MSINGI WA SOMO HILI**

Tutajifunza katika somo hili jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi maishani mwa watu. Je! unakumbuka jinsi tulivyojifunza katika sura zilizopita za kitabu hiki kwamba Roho ni nani na wakati alipooanza kazi yake ulimwenguni? Utajifunza leo yale anayotaka waamini wafanye ili awatumie na kile kitakachozuia kazi yake kufanyika.

Ni lazima turudi kwa kitabu cha Mwanzo ili tujifunze habari za Roho Mtakatifu. Tunasoma kwamba alikuwepo wakati ulimwengu na watu wake walipoumbwa. Biblia inafundisha kwamba Roho alipita juu ya viumbe vyote akifanya mapenzi ya Mungu. Roho ni sehemu yenye uwezo sawa katika utatu.

Roho Mtaktifu alitabiri kuzaliwa kwa Yesu. (Luka 1:35) Alikuwepo wakati wa kubatizwa kwake. (Mathayo 3:13-17) Alipanga kuanza kwa huduma ya Yesu na akamwezesha kufanya miujiza. Alimwongoza kuhubiri na kufundisha na akamhudumia wakati alipojaribiwa nyikani. Mwishowe, Roho alimfufua Yesu katika wafu.

Maneno na kazi ya Yesu viliongozwa na Roho. Watu walistaajabu jinsi Yesu alivyofanya miujiza yake walisema kwamba anatumia uwezo wa Shetani. Lakini Yesu alisema kwamba alifanya miujiza hiyo kwa uwezo wa Roho wa Mungu. (Mathayo 12:28)

Mtu hawezi kuwa Mkristo bila ya uwepo wa Roho Mtakatifu. Wanadamu huwa wamekufa kiroho mpaka wanapofanywa upya na Roho Mtakatifu. Tusisahau kwamba Mungu Mwana



KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu jinsi Shetani anavyotumia uchawi kufanya kazi yake.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Mtafute mshiriki wa kanisa lako ambaye amewahi kushiriki katika uchawi atoe ushuhuda kwa dakika tatu.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Utajifunza kuhusu uchawi na kazi ya Shetani katika somo hili. Utajifunza jinsi ya kuitikia uchawi katika jamii yako.

Watu wengi siku hizi huuendea uchawi wanapopata shida. Shida hiyo inaweza kuwa ugonjwa, matatizo ya jamaa au kuhitaji pesa. Watu wengine huundea uchawi ili kutengeneza maisha ya baadaye.

Watu huwa hawajui kwamba uchawi ni kazi ya Shetani. Shetani hutumia uchawi kutimiza kusudi lake. Mwandishi wa Yohana anatuambia kwamba Shetani huja kuiba, kuua na kuharibu. (Yohana 10:10)

Wale wanaojihusisha na uchawi hata ukiwa kidogo huvutwa nao. Mwishowe hufa kiroho. Hutenganishwa na Mungu. Biblia inaita kutenganishwa huku na Mungu, mauti. Watu hao watakuja kuangamizwa na Shetani. Hawataurithi ufalme wa Mungu. (Wagalatia 5:20-21)

Soma 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6. Mwandishi anatuambia habari za Manase, mfalme wa Yerusalemu. Manase alifanya maovu mbele za Mungu. Tunaambiwa katika kifungu cha 6 kwamba alimchoma mwanawe kwa kuitolea miungu sadaka. Alishiriki katika uaguzi, ubashiri na uchawi. Aliwaendea pia na walozi. Manase aliamini nguvu za uchawi badala ya Mungu.

Kutoka 22:18 inatuambia kwamba tusiwaruhusu wachawi au walozi waishi kati yetu. Wanaweza kuyaharibu maisha yetu kwa mtindo wao wa maisha.

Soma Matendo 16:16-18. Paulo alizungumzia kuhusu kijakazi mmoja aliyekuwa na roho (pepo) wa uaguzi. Watu walimtumia kijakazi huyu kupata pesa. Pepo aliyekuwa ndani yake alimtambua Paulo na wenzake kuwa watumishi wa Mungu. Aliwafuata akipiga kelele na kuwashangaza watu waliokuja kusikia mahubiri. Paulo alikasirika na akamkemea pepo huyo amtoke. Nguvu za Mungu zilionesha kuwa na uwezo mkuu kuliko za Shetani.

Soma 2 Wakorintho 11:13-15. Biblia inatwambia jinsi Shetani anavyojigeuza na kuwa malaika wa nuru. Hujivunia kazi yake, nguvu na wajibu. Wale wanaomwabudu hujibadilisha na kudai kwamba ni mitume wa Yesu Kristo. Shetani hutumia nguvu na uwezo wake kufanya ishara na miujiza ya kuwafanya watu wamwamini. Walio dhaifu katika imani huvutiwa mara moja.

Watu wanapaswa kujua kwamba Mungu ametoa kupitia kwa Yesu mambo wanayotafuta katika uchawi. Tunapaswa kumwamini Mungu kututimizia shida zetu zote. Anawaahidi matumaini watoto wake. Kusudi lake ni kwa kila mtoto wake apate uzima wa milele. Anajua kwamba Mungu anatujali. Anatutakia mema. Kwa hiyvo hatupaswi kuamini wala kuogopa uchawi.

**KULIFUNDISHA SOMO**

**UTANGULIZI**

Mwambie mtu uliyemwalika atoe ushuhuda wake sasa. Atapaswa kusema jinsi alivyoshiriki na sababu iliyomfanya aache uchawi. Andika mambo muhimu anayosema. Tazama hadithi ya Rachel kutoka Utangulizi wa vitabu vya wanafunzi.

Uliza: "Je! Rachel anapaswa kuitikiaje shida hiyo? Je! kwa nini?" Wape muda wa kujibu.



Uliza: "Je! unaelewa kuja kwa Roho mtakatifu?" Wape muda wa kujibu na kuuliza maswali.

Sema: "Unaye Roho Mtakatifu. Alianza kuishi ndani yako ulipompekea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako. Anataka kumtukuza Kristo maishani mwako. Utapata furaha amani na furaha ukimruhusu akutumie. Roho atakufunulia mengi unapojitoa kwake kila siku. Ni lazima ukubali kwa imani uwepo wake. Hapo ndipo Kristo ataishi ndani yako kama Bwana."

**KUOMBA**

1. Waombee wanafunzi wako waelewe kusudi la Roho Mtakatifu maishani mwao.

2. Waombee wanafunzi wako wamtii Roho Mtakatifu aliye maishani mwao.

3. Omba kwamba kila mwanafunzi atashiriki katika huduma ya Kristo.

## SURA YA KUMI

# KAZI YA ROHO MTAKATIFU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Luka 1:35; Mathayo 3:13-17; Yohana 14:16-20; Warumi 8:6-14

VIFUNGU VYA LEO: Luka 1:35; Mathayo 3:13-17; Yohana 14:16-20; Warumi 8:6-14.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanzisha kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu" (Wafilipi 1:6).

Uliza: "Je! kwa nini Roho Mtakatifu huja?" Wape muda wa kujibu . Mwambie mmoja wao asome Matendo 2:21.

Sema: "Kazi ya kwanza ya Roho Mtakatifu katika maisha ya mtu ni kumthibitishia dhambi zake, na kumwokoa mtu ye yote anayempokea. Hatimaye Roho Mtakatifu huanza kufanya kazi ndani ya mwamini huyo kumwezesha kumtumikia Bwana. Roho huwabariki wengine kupitia kwa yule aliyeokoka. Huwathibitishia wengine uovu wao, dhambi na hukumu.

"Kusudi la Roho Mtakatifu ni kumtukuza Mungu kupitia kwa mwanawe, Yesu Kristo. Mungu Baba na Roho Mtakatifu wanamshawishi kila mtu amheshimu Mwana, Yesu Kristo. Roho Mtakatifu hutusaidia kumruhusu Yesu kutawala maisha yetu."

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Uliza: "Je! unawezaje kujua kwamba mtu amepokea Roho Mtakatifu?" Ngojea wajibu. Mwambie mwanafunzi mmoja asome Matendo 2:4 na mwingine Matendo 2:17-18.

Sema: "Vifungu hivi vinaelezea mambo ambayo Roho huwafanyia watu. Huwapa uwezo wa kunena Neno la Mungu kwa ujasiri. Huwapa uwezo wa kufanya kazi njema. Hutusaidia kumshuhudia Kristo na kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu. Roho Mtakatifu hutusaidia kuelewa habari njema, na kuitikia kwa imani.

"Roho Mtakatifu huja kuishi ndani yetu tunapotubu dhambi zetu na kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Atawajaza wote wanaomtafuta. Humwokoa kila mtu anayempokea. Humfariji, humwongoza na kumfundisha kila mwamini. Hufanya kazi ndani yetu kutusaidia kumtumikia Bwana Yesu. Huwabariki watu wengine kupitia kwetu."



Sema: "Uchawi upo katika jamii zetu. Tunapaswa kujua yale Biblia isemayo kuhusu uchawi."

**MAELEZO**

Mwambie mwanafunzi mmoja asome 2 Mambo ya Nyakati 33:1-6. Sema: "Uchawi umelezwa katika fungu hili kama kaumini na kuheshimu vitu au watu badala ya Mungu. Uaguzi, ulozi, hirizi, pepo (kuzimu) vyote ni sehemu ya uchawi.

"Mtu anapoamini mambo haya, huwa anaamini kazi ya Shetani. Hii ndiyo sababu Biblia inakataza aina yo yote ya uchawi."

Wachague wanafunzi watatu wasome vifungu hivi: Kutoka 22:18, Mika 5:12, Wagalatia 5:20-21. Mwambie mwingine asome Matendo 16:16-18.

Sema: "Kijakazi huyu alikuwa akifanya uaguzi kwa nguvu za pepo aliyekuwa ndani yake. Paulo alimkemea yule pepo kwa jina la Yesu Kristo, naye akamtoka."

Uliza: "Je! unajifunza nini kutoka kwa hadithi hii?" Ngojea wajibu.

Sema: "Fungu hili linatuambia kwamba waamini wana uwezo juu ya kazi ya Shetani."

Uliza: "Je! inamaanisha nini kusema '... kwa jina la Yesu...'?" Wape muda wa kujibu. Waambie waangalie majibu katika vitabu vyao.

Mwambie mwanafunzi ambaye hajasema cho chote asome 2 Wakorintho 11:13-15.

Sema: "Tunasoma katika vifungu hivi kwamba Shetani hujigeuza kuwa mfano wa malaika wa nuru. Mfano huu unatupa ukweli fulani kuhusu uchawi. Hutokea ili kuwavuta

watu. Kusudi la uchawi ni kutimiza mapenzi ya Shetani katika maisha ya watu."

## UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Shetani bado anafanya kazi hata sasa. Hutumia uchawi, kuzimu, uaguzi, ulazi, ubashiri, manabii wa uongo, na uongo kutimiza kusudi lake. Kusudi kuu la Shetani ni kuharibu maisha ya watu.

"Shetani hutumia watu wanaopendezwa na kazi yake, marafiki, majirani na hata jamaa zetu kutuelekeza katika mauti. Hutushawishi tuwaamini na mienendo yao ya uovu. Shetani huhakikisha kwamba amewapotosha watu na Mungu ili wafe katika dhambi. Hataki watu wamwamini Yesu Kristo na waokoke.

"Shetani hututenganisha na Mungu kwa kutudanganya. Twaona jinsi alivyomdanganya Hawa katika bustani ya Edeni (Adeni). Alitumia kitu cha kupendeza, tunda, kumfanya Hawa amshuku Mungu. Akamwambia, '...Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya' (Mwanzo 3:4-5). Adamu na Hawa walijua mema na mabaya walipokula tunda hilo, lakini wakafa kiroho."

Sema: "Baadhi ya watu siku hizi wana ushirikina na ishara ambazo huzitii na kuziogopa. Wameamini sana mambo haya mpaka hawawezi kuona nguvu za Yesu Krsito. Hata baadhi ya Wakristo wanashiriki katika Ukristo na uchawi. Hufuata na kumwabudu Kristo wanapofurahia maisha, lakini hukimbilia uchawi wanapopatwa na shida. Hawajui kwamba Yesu Kristo ana uwezo wa kuwaondolea shida zao.

"Watu wanapaswa kujua kwamba wamewekwa huru na mambo haya yote. Yesu alituweka huru kwa kufa msalabani.



uwezo wa Mungu, lakini ni lazima tuamue kama tutamruhusu afanye kazi maishani mwetu."

## MAELEZO

Sema "Yohana 16:7-13 inatwambia kwamba Yesu aliahidi kuwaachia wanafunzi mfariji. Aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu awe pamoja nao. Roho alikuwepo tangu mwanzo, lakini alikuwepo kwa watu maalum ambao Mungu alichagua. Wakati huu angekuwepo ndani ya kila mwamini.

"Tunasoma katika kifungu hiki yale ambayo Roho Mtakatifu atafanya. Angewapa wanafunzi uwezo wa kufanya kazi yao. Angewasaidia wamshuhudie Kristo na kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu. Angewawezesha kumwelewa Mungu vizuri. Angewasaidia wamwitikie Mungu kwa imani. Angewaonyesha wapotevu dhambi zao. Angewaonyesha watu haki na hukumu ya Mungu. Angewasaidia waelewe maana ya kuteswa kwa Kristo, kufa na kufufuka kwake. Angewaongoza watu kujua ukweli wote unaohusu wokovu."

Sema: "Yoeli 2:28-32 inatuambia kwamba Roho atatolewa kwa miili yote. Ingefanyika hivyo wakati maalum. Litakuwa tendo maalum. Roho angekuja kuishi ndani ya watu wa Mungu.

"Matendo 2:14-21 inatuambia kuhusu utimilifu wa unabii wa Yoeli 2:28-32. Hii ilifanyika siku ya Pentekoste. Roho Mtakatifu alikuja kama uvumi mkuu. Aliwajia waamini wote wa siku hiyo. Alikuja kuishi ndani ya kila mwanadamu.

"Roho aliwapa wanafunzi uwezo siku hiyo. Walinena kwa lugha. Petro alihubiri kwa ujasiri na akawaelezea injili wote waliokuwepo. Kila mtu aliyekuwepo alisikia injili katika lugha yake mwenyewe. Watu wa kila taifa walionyeshwa upendo wa Mungu."

cha baraka kwa wale waliotubu na kipindi cha hukumu kwa wale waliomwasi Mungu. Ni wakati ambao ufalme wa Shetani utaangamizwa na ufalme wa Mungu. Silaha inayotumiwa kuangamiza ufalme Shetani ni upendo, msalaba na kufufuka kwa Yesu.

## KULIFUNDISHA SOMO

### UTANGULIZI

Uliza: "Je! kwa nini Roho Mtakatifu alikuja?" Waonyeshe swali hili ulioandika ubaoni, au kwenye karatasi kubwa. Utapata majibu kama kuwathibitisha wanadamu dhambi zao, kuwaongoza waamini katika ukweli wote. Kuwepo pamoja na mwamini na kuleta njia mpya ya Mungu kushirikiana na mwanadamu. Andika majibu yao. Wasome Yohana 16:7-13 na Matendo 2:14-21. Waulize wanafunzi waseme kazi ya Roho katika kila fungu. Andika sababu hiyo ubaoni kama haijaandikwa.

Uliza: "Je! tunapata matumizi gani kwa umeme?" Wahimize wanafunzi waseme matumizi ya umeme. Sisitiza umuhimu wa umeme.

Sema: "Watu wengi hawajui jinsi umeme unavyokuja nyumbani kwao, lakini wanaweza kuona matumizi yake. Hutumiwa kufanya kazi nyingi. Watu ambao hawana umeme hawawezi kujua matumizi yake. Wao husikia tu habari zake. Ndivyo ilivyo na watu ambao hawana Roho Mtakatifu. Hawawezi kuelewa jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi.

"Mtu hupokea Roho Mtakatifu mara tu anapompokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake. Roho huanza kuishi ndani yake. Ni ghali sana kuleta umeme nyumbani kwetu. Lakini tunaweza kuupata tuko tayari kulipa gharama hiyo. Hapo ndipo tutaanza kuutumia. Roho huja kuishi ndani yetu tunapompokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. Yeye ni



Alitusafisha kwa damu yake. Atungojea tutubu dhambi zetu na tumwombe msamaha.

"Mungu amekataza uchawi. Mauti ndiyo adhabu ya watu wanaomkataa Mungu. Hakuna shida kuu ambayo Mungu hawezi kuitatua. Ana uwezo na nguvu kuu kuliko Shetani. Wakristo wana ushindi wa Mungu kwa sababu ameshinda ulimwengu. Tunapaswa kumwamini Mungu kwa shida zetu zote. Tukumbuke kwamba Mungu anatutakia mema maishani."

Uliza: "Je! utamwamini Mungu leo na umpolekee mizigo yako?"

Sema: "Jaribu kufuata njia ya Mungu, naye atayabadili maisha yako. Tumejifunza leo kwamba Shetani hutumia uchawi kutimiza kusudi lake. Kusudi la Shetani ni kuharibu maisha ya watu. Tumejifunza pia kwamba Mungu amekataza uchawi. Tunapaswa kumtegemea Mungu kututatulia shida zetu. Mungu anatutakia mema."

### KUOMBA

1. Andika mambo kumi ambayo Mungu amekufanyia. Mshukuru kwa kukupa vitu hivyo.

2. Mwombe Mungu akusamehe kama umewahi kujihusisha na uchawi.

3. Choma hirizi zo zote au vifaa vingine vya uchawi kama unavyo, na watie mioyo wa wanafunzi wako kufanya hivi pia.

## SURA YA TANO

# JINSI YA KUTAMBUA UCHAWI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Yeremia 27:5-9; Danieli 2:27-28; Isaya 2:5-6; 1 Yohana 4:1-6

VIFUNGU VYA LEO: Yeremia 27:5-9; Danieli 2:27-28; Isaya 2:5-6; 1 Yohana 4:1-6

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Basi matendo ya mwili ni dhahiri,...uchafu,...uchawi,...watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu" (Wagalatia 5:19-21).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu jinsi ya kutambua uchawi.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Tafuta vifaa vinavyotumiwa kwa uchawi pale unapoishi na uvilete darasani. Lete pia dawa za kienyeji (mzizi, majani, maganda ya mti) zinazotumiwa katika jamii yako.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Unaweza kutambua uchawi kulingana na matokeo yake. Huwafanya watu waamini sanamu. Hutufanya tuwe adui wa Mungu na huleta chuki kati ya watu. Mungu amejifunua kwetu katika Yesu Kristo. Mtu ye yote anayekataa kumtambua Yesu kuwa Mwana wa Mungu na anayekataa mamlaka yake ni wa Shetani. Ni muhimu kujua kwamba Shetani hutumia uchawi kutimiza lengo lake. Shetani huja kuiba, kuua na kuharibu maisha ya watu. Hutumia uongo, uchafu, uaguzi na miujiza kutimiza lengo lake. Wachawi hudai kuwa na nguvu maalum. Hudai kwamba wanaweza kutatua shida za maisha. Hudai kuwapa watu vitu wanavyotaka.



wanafunzi wake yale ambayo yatampata. Aliwaambia kwamba atakufa na atawacha na kwenda kwa Baba. Lakini hatawaacha peke yao. Aliwaahidi kumtuma Roho Mtakatifu awe pamoja nao. Wanafunzi walisikitika sana waliposikia habari hii. Walimwuliza Yesu kule anakoenda. Yesu akawaambia, "...yawafaa ninyi mimi niondokee, ...mimi nikienda zangu nitampeleka kwenu" (Yohana 16:7).

Wanafunzi walifikira kwamba kifo cha Yesu kingekuwa mwisho wa huduma yake. Yesu aliwahakikishia faida ya kuondoka kwake. Kwanza, kuondoka kwake kulimaanisha kufa msalabani na kwenda kwa Baba. Pili, Roho Mtakatifu angekuja kukaa ndani yao na kufanya kazi. Tatu, Baba na Mwana wangekuwa pamoja nao kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Yohana 16:8 inasema, "Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi na haki, na hukumu." Roho Mtakatifu angewasaidia wanafunzi kumshuhudia Kristo na kuhubiri injili ya Ufalme. Roho angewasadia wapotevu kuelewa injili na kuiamini.

Yohana 16:13 inasema, "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; ...na mambo yajayo atawapasha habari yake." Kazi nyingine ya Roho ingekuwa kuwawezesha wanafunzi kuelewa maana ya kifo cha Yesu kuteseka, na kufufuka. Wangeelewa ukweli mwingine unaohusu wokovu.

Matendo 2:17-18 inasema, "Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, ...nao watatabiri." Petro aliamini kwamba siku za mwisho zilianza wakati wa Pentekoste. Mungu alileta Roho Mtakatifu siku hiyo. Siku za mwisho hazikumaanisha mwisho wa ulimwengu, zilimaanisha kipindi cha mwisho ambapo Mungu alishiriki na watu wake kwa njia maalum. Kilikuwa kipindi kilichodhihirisha uwepo we Roho Mtakatifu. Kilikuwa kipindi

kutawala maisha yetu. Atatusaidia kuelewa na kumjua Mungu. Mungu atakuongoza unapopanda Neno lake moyoni mwako."

**KUOMBA**

1. Panga wakati wa kusoma na kutafakari Neno la Mungu kila siku. Chagua kitabu au jambo la kujifunza. Tafuta mpango ambao utakutia moyo na kukufanya uone maendeleo yako.

2. Jitoe kutii Neno la Mungu.

3. Jitoe kukariri kifungu kimoja kila wiki.

4. Mwombe Roho Mtakatifu akuongoze kila wakati unaposoma Maandiko.

## SURA YA TISA

# KUJA KWA ROHO MTAKATIFU

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Yohana 16:7-13; Matendo 2:14-21

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 16:7-13; Matendo 2:14-21

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Na itakuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa" (Matendo 2:21).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu maana ya kuja kwa Roho Mtaktifu maishani mwao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Andika swali hili ubaoni au kwenye karatasi kubwa: Je! kwa nini Roho Mtakatifu alikuja?

**MSINGI WA SOMO HILI**

Yohana alipoandika Injili hii, alizungumzia pia jinsi Yesu alivyowafundisha wanafunzi wake. Yesu aliwafundisha



Tutasoma leo Maandiko yanayohusu kazi na lengo la Shetani ili tuweze kutambua uchawi.

Yesu aliwaamuru Israeli katika Yeremia 27:5-9 kujitoa kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli. Mungu alimchagua Nebukadreza kuwa mtumishi wake. Mungu alimpa mamlaka na mataifa yote yalipaswa kumtumikia mpaka Mungu atakapomfanya Nebukadreza awatumikie.

Mungu aliendelea kuwaonya watu wasiwasikilize manabii wao, wabashiri, wanaota ndoto, watambuzi au waganga. Watu hawa waliwakataza Waisraeli wasimtumikie mfalme wa Babeli. Ulikuwa mpango wa Mungu kumpa Nebukadreza mamlaka. Mungu alikuwa na uwezo wa kusema, kufanya au kubadili jambo lo lote. Alitaka Israeli wamtii badala ya kumtii mwanadamu.

Tunasoma katika Danieli 2:27-28 jinsi mfalme Nebekadrneza alivyoota ndoto. Alifadhaika sana wala hakuweza kulala. Aliwaita wazee wenye hekima, waganga na wachawi wa Babeli kutafsiri ndoto hiyo, lakini wakashindwa. Alikasirika sana na akataka kuwaangamiza. Lakini Danieli, mtu wa Mungu, alimwambia mfalme tafsiri ys ndoto hiyo.

Mungu alimfunulia Danieli maana ya ndoto ya mfalme. Mfalme aliwaambia sana wazae wenye hekima, waganga, wachawi na wabashiri, lakini walishindwa. Mungu alikuwa na uwezo wa kumfunulia mfalme ukweli.

Soma Isaya 2:5-6. Tunaona jinsi Mungu alivyowakataa watu wa nyumba ya Yakobo, kwa sababu walishiriki na wabashiri na waaguzi. Waisraeli walimwasi Mungu na kuamini nguvu za pepo. Isaya aliwaambi warudi kuenenda "...katika nuru ya Bwana" (Isaya 2:5). Mungu alikuwa tayari kuwasamehe na kuwakubali kama walikuwa tayari kumtii na kumwamini.

Mungu alitaka Israeli waamue. Wangemtii na kuishi au wamkatae na wafe kwa upanga.

## KULIFUNDISHA SOMO

### UTANGULIZI

Mwambie mwanafunzi mmoja asome hadithi ya Simoni kutoka katika kitabu chake.

Uliza: "Je! utafanya nini ukiwa katika hali ya Simoni?" Mpe nafasi ye yote anayetaka kujibu. Toa muhtasari wa majibu yao.

Uliza: "Je! unawezaje kutofautisha uchawi na madawa ya kienyeji? Je! wachawi hudai kufanya nini?" Wape muda wa kujibu. Andika majibu yao ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

Uliza! "Je! uchawi hutimiza madai haya?"

Sema: "Tumesema kwamba uchawi ni kazi ya Shetani. Shetani hufanya cho chote kutimiza lengo lake."

Uliza: "Je! Shetani hutumia madai haya kutimiza lengo lake?" Ngojea wajibu.

Sema: "Watu wataweza kutambua uchawi wanapoona madhara yake. Yesu alisema kwamba unaweza kujua waalimu wa uongo kwa matunda yao. Ndivyo ilivyo na uchawi. Utajua uchawi kwa matunda yake."

Waambi wanafunzi watatu waseme jinsi wawezavyo kutofautisha uchawi na madawa ya kienyeji.

### MAELEZO

Sema: "Hatuwezi kuelewa uchawi bila ya kujua watu wanaofanya. Hebu tuzungumzie juu ya wachawi, walozi na kuzimu. Tutazungumzia pia waganga wa kienyeji.



Hutusaidia kumpokea Kristo maishani mwetu na kuenenda naye kila siku."

### UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Uliza: "Je! kuna mamlaka yo yote juu ya maisha na matendo yetu? Je! ni yapi na ni kwa nini?" Hakikisha wanaelewa kwamba Maandiko ni mamlaka kwa maisha yetu kwa sababu ni Neno la Mungu.

Uliza: "Je! tunawezaje kuelewa Maandiko vizuri?" Wape muda wa kujadiliana na kuuliza maswali.

Sema: "Neno la Mungu lina mafundisho kwa maisha yetu. Kwa hivyo tunapaswa kuliweka mioyoni mwetu kwa kulisoma, kulikariri na kulitafakari."

Mwalimu, eleza sasa jinsi unavyofanya tendo hili maishani mwako. Unaweza kutumia vitu kama vifungu unavyokariri au wakati wa kimya na Mungu. Waonyeshe kifaa cho chote ulicholeta cha kukusaidia kufundisha somo hili. Waambie kuhusu makundi ya kujifunza Biblia unayohudhuria.

Sema: "Biblia ni kitabu muhimu sana kwa Mkristo. Hakuna kitabu kingine duniani kama Biblia. Ni taa ya miguu yetu na mwanga wa njia yetu. (Zaburi 119:105) Ni Neno lenye pumzi ya Mungu.

"Tunaweza kuongozwa kumtumikia Mungu kwa kusoma Biblia. Roho Mtakatifu huendelea kufanya kazi maishani mwetu na ulimwenguni. Hutusaidia kuelewa Biblia na mapenzi ya Mungu maishani mwetu.

"Tunapaswa kusoma na kuyatafakari Maandiko. Hivyo ndivyo yanayoweza kufanya kazi maishani mwetu. Tunapaswa kumruhusu Roho Mtakatifu atuongoze katika kutambua ukweli wa Maandiko. Lakini ni lazima kwanza Yesu Kristo awe Bwana na Mwokozi wetu kabla Roho Mtakatifu kuanza

Mwambie mwanafunzi mmoja asome 2 Timotheo 3:14-17. Uliza: "Je! kuna jambo lo lote katika fungu hili ambalo linatuonyesha kwamba Biblia ni tofauti na vitabu vingine?" Wape muda wajibu. Eleza maana ya kuongozwa au "pumzi ya Mungu" kulingana na uhusiano wake na Biblia. Tazama Msingi wa Somo Hili. Mwambie mwanafunzi mmoja asome 2 Petro 1:19-21 ili uweze kuwaeleza zaidi.

Sema: "Biblia ni Neno la Mungu. Ina mamlaka juu ya maisha yetu. Tunapaswa kutii yale inayosema. Tukikataa kutii tutakosa baraka za Mungu maishani mwetu. Pia, huwa tunaadhibiwa kwa kukosa kutii."

**MAELEZO**

Uliza: "Je! Maandiko yana faida gani kwetu?" Wape muda wa kujibu.

Sema: "Neno la Mungu hutupa ukweli na huongoza maisha yetu. Huwa tunasoma Maandiko ili tumfahamu Bwana wetu vyema na tushiriki naye. Maandiko yanafaa kwa mafundisho, kuonya, kuongoza na kuadibisha katika haki. Hutukamilisha tupate kutenda kila tendo jema. Hutusaidia kuona dhambi zetu, kukiri na kumwendea Mungu.

"Maandiko huwaongoza watu kumwabudu Mungu na kutambua ukweli wake. Mungu hutumia Neno lake kutuongoza. Hutupa Roho Mtakatifu anayetusaidia kumwelewa. Hunena nasi kupitia kwa Neno lake, Biblia. Mungu ndiye aliyeonza uandishi wa Biblia. Alipanga, akachagua na akaongoza wanadamu kuiandika Biblia ni Neno la Mungu kwetu.

Mtu hawezi kumtambua Mungu au ukweli wake kimakosa. Mungu hujidhihirisha kwetu kupitia kwa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hutuongoza kumjua na kumwelewa Mungu.



Wachawi na walozi hudai kuwa na uwezo wa kuponya na kuloga watu. Wale wa kuzimu hudai kuwa na uwezo wa kuwasiliana na pepo. Waganga wa kienyeji hudai kuponya kila aina ya ugonjwa kwa kutumia mizizi, shina za mimea na majani fulani.

"Wachawi huwa wanajifunga shuka ndefu. Huvaa ushanga shingoni zilizofungwa mifupa, pembe na shanga. Wakati mwingine huvaa kama watu wengine.

Wachawi hudai kuponya kila aina ya magonjwa. Hutumia mizizi, shina za mimea na mimea kama dawa yao. Hudai kwmba wana uwezo juu ya kila kitu. Huamini roho na pepo. Huwaambia watu kwamba shida na mikasi yao huletwa na pepo wanaowazunguka.

"Wakati mwingine walozi hufanya kazi yao usiku. Huwatembelea na kumhudumia mtu ye yote anayewaendea.

"Wanaohusika na kuzimu huvaa shuka nyeusi na shanga shingoni, au wanaweza kuvaa kama watu wengine. Husema kwamba wanaongozwa na pepo ambao humwendea wakati mtu, jamaa au kijiji wanapopatwa na mikosi au janga. Wao hudai kuwa na uwezo wa kuwatuliza pepo.

"Wanganga wa kienyeji ni kama madaktari. Hutayarisha mizizi, mashina ya miti, majani ya mimea kama dawa ya kutibu wagonjwa wao. Hawatumii uchawi wala kudai kwamba wanajua chanzo cha mikosi na shida za maisha. Wengi wao hawajihusishi na roho wala pepo. Huwapa madawa watu wanaoenda kuwaona."

**UKWELI KATIKA MAISHA YETU**

Sema: "Uchawi ni kazi ya Shetani. Hutumia uchawi kuwadanganya na kuwafanya watu wamwamini. Uchawi ni pamoja na uaguzi, ubashiri na ulozi. Mambo haya hufanywa na

watu walioamua kumfuata na kumfanyia Shetani kazi. Si lazima ukae chini na kuamua kumfuata Shetani. Pengine mtu huwa hajakata shauri la kumfuata Yesu, na ndipo huingia katika mtego wa Shetani.

"Uchawi husababisha kutoelewana, kutoaminiana na chuki kati ya watu. Huwafanya watu waamini sanamu na miungu badala ya Mungu Baba. Watu wanaoshiriki katika uchawi husema wana uwezo wa kuponya, kuloga na kutatua shida na mikosi ya maisha. Hii si kweli!

"Shetani anatumia uchawi kuwafanya Wakristo wasimwamini Mungu. Shetani anapigana vita ambavyo Mungu tayari ameshinda. Hakunà uwezo na nguvu za kuushinda uwezo wa Mungu."

Uliza: "Je! Mungu anafurahia uchawi?" Wape muda wa kujibu.

Sema: "Mungu anakataa aina yo yote ya uchawi. Aliwaonya Israeli wasiwasikilize watu kama hawa. Anatuonya sisi hata sasa. Anataka tumwamini yeye pekee. Mungu anatuita tuenende "...katika nuru ya Bwana" (Isaya 2:5) na tumtumikie. Tunaweza kumwelewa Mungu na kazi yake maishani mwetu kama tu ndani yake.

"Uchawi, ulozi na kuzimu haviwezi kututimizia mahitaji yetu kwa sababu unahusiana a pepo wachafu. Mungu hawezi kukosa kututimizia tunapomwamini.

"Yesu ndiye mfano wetu jinsi ya kuishi. Alimtii Baba aliyemtuma. Nasi tunapaswa kumtii Yesu na kukemea hila na udanganyifu wa Shetani. Yesu alikuja ili wale wanaomwamini wawe na uzima wa milele Shetani hutaka kuharibu maisha ya watu. Mungu anataka kukutoa katika nguvu za Shetani na uchawi."



kwa ushirika kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu hakumwacha mwanadamu alipofanya dhambi. Mungu aliamua kuonyesha upendo wake kwa mataifa yote akitumia Israeli kama wateule wake. Tunaona dhihirisho la upendo huu katika Yesu Kristo aliyefia dhambi za ulimwengu wote.

2 Timotheo 3:14-17: Fungu hili linaonyesha kwamba Maandiko humshauri mwanadamu jinsi ya kupata upendo wa Mungu wa ukombozi. Maneno yenye pumzi ya Mungu ni mamlaka na yanafaa kwa mafundisho, kuonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwaadibisha katika haki. Hakuna kiwango kwa yale ambayo Neno la Mungu laweza kufanya maishani mwetu. Paulo alithibitisha jambo hili. Alitwambia kwamba mtu hukamilika wakati anapoongozwa maishani na Neno la Mungu. Huwa tayari kwa kila kazi njema. Wewe kama mwalimu huwa kamili unaposoma Neno la Mungu na kulitumia maishani.

2 Petro 1:21: Petro anasema mambo mawili muhimu katika Maandiko haya. Kwanza, Maandiko si maneno ya wanadamu. Wanadamu hawakujiwa na mawazo ya kuandika maneno haya. Waliongozwa na Roho Mtakatifu kunena na kuandika. Pili, Maandiko hayawezi kuelezwa na mwanadamu ila na mwandishi mwenyewe au Roho Mtakatifu aliyewaongoza kuandika.

## KULIFUNDISHA SOMO

### UTANGULIZI

Shika katika mkono mmoja vitabu ulivyoleta na Biblia katika mkono mwingine.

Uliza: "Je! kuna tofauti gani kati ya vitabu hivi?" Jaribu kujua ufahamu wa wanafunzi wako juu ya ukamilifu na mamlaka ya Biblia kwa kuwauliza maswali.

SURA YA NANE

# ROHO MTAKATIFU NA UONGOZI

**KUJITAYARISHA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: 2 Timotheo 3:14-17; 2 Petro 1:12-21

VIFUNGU VYA LEO: 2 Timotheo 3:14-17, 2 Petro 1:19-21

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongonzwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:21).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawaonyesha wanafunzi wangu mamlaka na umuhimu wa Maandiko maishani mwao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Njoo darasani na vitabu viwili au vitatu vya kawaida, vifungu vya kukumbuka au vifaa unavyotumia kukukumbusha Maandiko, na mpango wa kujisomea Biblia.

**MSINGI WA SOMO HILI**

Biblia ni mamlaka ya maisha yetu. Ni Neno lililoletwa na Mungu. Neno hili la Kiyunani, uongozi, (2 Timotheo 3:16) maana yake ni "pumzi ya Mungu." Mungu Roho Mtakatifu aliongoza wanadamu kuliandika. Walitumia hekima yao kuliandika Neno hili bila kosa. Biblia iliandikwa kwa kipindi cha miaka 1500. Kila kitabu kiliandika wakati tofauti.

Biblia inazungumzia juu ya jambo moja. Ina mpango wa lengo moja. Kiini hasa cha Biblia ni upendo wa Mungu wa kumkomboa mwanadamu. Kiini hiki kinaweza kufuatwa kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Tunaona katika Mwanzo jinsi mwanadamu alivyoanguka. Mwanadamu alimuasi Mungu katika bustani ya Edeni. Matokeo yake yalikuwa kuvunjika



Waambie wanafunzi wamfikirie mtu wanayejua kwamba anashiriki katika uchawi. Waongoze kumwombea mtu huyu Mungu apate kumwokoa. Wahimize wamwombe Mungu awape nafasi ya kumwonya mtu huyo juu ya hatari ya uchawi.

**KUOMBA**

1. Mwombe Mungu akusaidie kufundisha somo hili.

2. Omba kwamba wanafunzi wako wataelewa ubaya wa uchawi.

SURA YA SITA

# UCHAWI NA MKRISTO

**KUJITAYARISHGA KUFUNDISHA**

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 18:10-12; Amosi 3:3; Mika 5:12; Marko 5:1-13; Matendo 8:9-24; 13:6-11; Waefeso 6:10-17

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 18:10-12; Marko 5:1-13; Matendo 8:9-24; 13:6-11; 16:16-18; Waefeso 6:10-17

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani" (Waefeso 6:11).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu jinsi Wakristo wanavyopaswa kujitenga na uchawi.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki au karatasi kubwa. Andika kichwa hiki: Uchawi na Mkristo.

## MSINGI WA SOMO HILI

Musa ndiye anayefikiriwa kuwa mwandishi wa Kumbukumbu la Torati. Waisraeli, watu wa Mungu, wamekubaliwa na matakwa ya amri za Mungu.

Kumbukumbu la Torati 18:10-12: Sehemu hii ina maonyo makali kuhusu ulozi na kubashiri. Mungu amewaamuru watu wake wajitenge na uchawi.

Kifungu cha 10: Kifungu hiki kinaonya kwamba pasiwepo na mtu ye yote wa kutoa wanawe kama dhabihu ya kuchoma au sadaka au mtu ye yote wa kushiriki katika uchawi. Mambo haya humchukiza Mungu. Mtu awapo Mkristo anapaswa kuacha kabisa aina yo yote ya uchawi. Yesu atamtunza.

Marko 5:6-13: Yesu alikutana na pepo, malaika wa Shetani, wakati wa huduma yake pepo hao walilia kwa sauti kuu walipokutana na Yesu. Yesu aliwakemea pepo hao wachafu, na wakamtoka mtu yule mara moja.

Katika Matendo 8, Petro alimkemea mtumishi wa Shetani aliyehubiri uwezo wa Yesu. Petro alimsihi atubu na aombe msamaha. Alimwambia ajitoe kwa Kristo na uwezo wake. Hupaswi kubabaishwa na uchawi ukiwa u Mkristo. Wala usiwe na matumaini yenye mashaka.

Katika Matendo 13:16-18, Paulo alimpinga mtumishi wa Shetani hapo Pafo. Paulo alijazwa Roho Mtakatifu, akamkemea mtu huyu na akawa kipofu.

Matendo 16:16-18 inatuambia kwamba Paulo alikuwa Filipi. Kijakazi (mtumwa) aliyekuwa na pepo wa uaguzi alianza kuchafua mahubiri ya Neno la Mungu. Paulo alimkemea na Pepo mchafu akamtoka. Yesu Kristo ndiye mwenye uwezo pekee. Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani ya wafuasi wa Yesu Kristo.



## UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Biblia inatufundisha kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya roho ya kila Mkristo. Roho wa Mungu huingia ndani ya Roho ya mtu anapozaliwa mara ya pili. Mtu huwa si Mkristo kama hana Roho Mtakatifu moyoni mwake. Warumi 8:9 inasema, '...Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.'

"Kuna tofauti kati ya kujazwa na Roho na Roho Mtakatifu kukaa ndani ya mtu. Mungu anataka tumpe mioyo yetu ili atujaze na Roho wake. Atatuwezesha kumhudumia kama tuna Roho. Wakristo watasema Neno la Mungu kwa ujasiri baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu." Waambie wasome Matendo 4:31.

Sema: "Mungu yuko tayari kujaza mioyo yetu na Roho wake. Lakini kabla ya kutujaza, ni lazima tutoe mioyoni mwetu mambo ambayo hayampendezi. Hapo ndipo tutauona ukuu wake maishani mwetu."

## KUOMBA

1. Omba kwamba wewe na wanafunzi wako mtaelewa kwamba Mungu amejidhirisha kwetu katika utatu.

2. Waombee wanafunzi wako wamruhusu Roho Mtakatifu atawale maisha yao.

3. Mwombe Mungu awasaidie wale wanafunzi ambao hawajampa Kristo maisha yao wafanye hivyo sasa.